HALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOBA

Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji

Simu: 028 2220287
Faksi: 028 2221839
E – MAIL:ded@bukobadc.go.tz

S.L.P. 491
BUKOBA

18 Februari, 2020

Unapojibu tafadhali Taja:
Kumb.Na.KGR/BDC/S.2/28/V/71

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba inatangaza nafasi za kazi kama ifuatavyo:

(1) KATIBU MAHSUSI III – NAFASI (01)

SIFA

i. Awe na elimu ya kidato cha IV au VI
ii. Awe na Mafunzo ya Uhazili na kufaulu mtihani wa Hatua ya tatu
iii. Awe amefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kiingereza Maneno 80 kwa dakika moja.
iv. Awe amepata mafunzo ya Kompyuta kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali, kwa Programu za Windows, Microsoft Office, Internet, E-mail na Publisher.
v. Awe na umri kati ya miaka 18 - 45
vi. Awe ni raia wa Tanzania.

MSHAHARA

Kwa kuzingatia ngazi ya mshahara wa Serikali, yaani TGS B kwa mwezi.

(2) MTENDAJI WA KIJIJI III – NAFASI (01)

SIFA

i. Awe na elimu ya kidato cha IV au cha VI.
ii. Awe na cheti cha Stashahada katika fani ya Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Maendeleo ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Uchumi na Mipango kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.
iii. Awe na umri kati ya miaka 18-45.
iv. Awe ni raia wa Tanzania.

MSHAHARA

Kwa kuzingatia ngazi ya mshahara wa Serikali, yaani **TGS B** kwa mwezi.

MAELEZO MUHIMU YA KUZINGATIA

i. Barua za maombi ziandikwe kwa mkono.
ii. Maombi yaambatane na vivuli vya vyeti (photocopies).
iii. Barua ziambatane na picha moja ya passport size.
iv. Mwombaji aambatishe CV na anwani ya mawasiliano kama Simu za mkononi, E-mail, Faksi nk.
v. Wale watakaoitwa kwenye usaili, watajigharamia usafiri na malazi.
vi. **Tarehe ya mwisho kupokea maombi ya kazi ni tarehe 04/03/2020.**

Barua za maombi zitumwe kwa anwani hii:

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya,
S.L.P 491,
BUKOBA.

LIMETOLEWA NA;

MKURUGENZI MTENDAJI

HALMASHAURI YA WILAYA BUKOBA